TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

# TAMKO LA MTANDAO WA WANAWAKE KATIBA, CHAGUZI, NA UONGOZI KUHUSU MISWADA ITAKAYOJADILIWA BUNGENI

## UTANGULIZI

Sisi wanamtandao wa **Wanawake, Katiba, Uchaguzi, na Uongozi** unaojumisha mitandao, mashirika na asasi za kiraia takribani 200, tunatoa tamko hili kwa lengo la kuujulisha umma wa Tanzania, wanaume kwa wanawake, kwamba tunadai kuingizwe **misingi ya usawa wa jinsia** kwenye miswada mitatu iliyowasilishwa Bungeni tarehe 10 Novemba 2023. Miswada hiyo ni Mswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani,2023, Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa, 2023 na Mswada wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, 2023.

Tamko hili linahusu madai yetu kwamba nchi yetu inatakiwa iwe na sheria zenye kubainisha usawa wa jinsia pamoja na kuanisha misingi ya uwajibishwaji kwa wale wote wanaopewa dhamana ya uongozi katika kutafsiri misingi hii katika sera na mipango mikakati ya utekelezwaji

Madai yetu haya yanaongozwa na misingi ya usawa wa kijinsia kama zilivyobainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Katika Katiba yetu Sehemu ya Tatu kifungu (12(1) kinasema, "Binadamu wote huzaliwa huru, na wote ni sawa" na Kifungu 13 (1-5) kinafafanua zaidi kwa kukataza aina zote za ubaguzi ikiwa ni pamoja na ubaguzi wa jinsia. Tunaamini kwamba ujenzi wa demokrasia shirikishi hauwezi kuimarika nchini kwetu kama misingi ya ubaguzi dhidi ya wanawake itaendelezwa na kuhalalishwa na sheria zinazotungwa.

Vilevile madai yetu tumezingatia misingi ya usawa iliyobainishwa katika mikataba na maazimio mbalimbali ya Kimataifa, kikanda, ambayo Tanzania imeridhia, Dira yetu ya Taifa 2025, ambayo imeweka lengo la kutokomeza aina zote za ubaguzi ikiwa ni pamoja na ubaguzi wa jinsia ifikapo mwaka 2025.

Pia tumekuzingatia muktadha wa sasa ambapo Tanzania kwa mara ya kwanza tangu tupate uhuru tumepata Rais mwanamke ambaye amedhamiria kuona nchi inaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya usawa wa kijinsia. Amekuwa akitekeleza azma hiyo kwa kuhakikisha nchi inakuwa na sera na mipango itakayowezesha watoto wa kike kupata haki sawa ya elimu kama watoto wa kiume. Pia Rais ameshiriki katika jukwaa la Umoja wa Mataifa la kizazi cha usawa wa jinsia (Generation Equality Forum) na amejitolea kusimamia utekelezwaji wa maazimio ya jukwaa hilo (Mfano kuwa kinara wa haki za kiuchumi- yaani Economic Justice and Rights action coalition as an accelerator to women's empowerment) na hapa nchini

tayari kuna mpango mkakati umewekwa wa kutekeleza maazimio ya jukwaa hilo katika ngazi ya taifa.

Muhimu zaidi, sisi wanamtandao wa Wanawake, Katiba, uchaguzi, na Uongozi, baada ya uchambuzi yakinifu wa miswada yote mitatu tumegundua mapengo ya jinsia katika miswada hiyo, na kwa pamoja tunadai mabadilko katika miswada hii ili kuwezesha kuwa na sheria zenye mrengo wa jinsia na zenye kuweka misingi ya uwajibishaji kwa wale wote wenye dhamana ya kusimamia na kutekeza sheria husika

## MAPENDEKEZO YETU

1) **Uteuzi wa Rais na Makamu wake**

Mswada wa Uchaguzi wa Rais, Wabunge, na Madiwani, 2023 Sura ya Tatu Kifungu cha 32 ubainishe usawa wa jinsia (50/50) kwa kuvitaka vyama vyote vyenye nia ya kushindania nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania viteue wagombea wawili yaani mgombea kiti cha Urais na Makamu wake. Endapo Mteule wa kiti cha Urais ni mwanamke, basi mgombea mwenza awe mwanaume au vinginevyo. Hoja yetu ni kwamba msingi huu wa usawa wa jinsia usipobainishwa basi baada ya kipindi cha Rais wa sasa kumalizika, huenda itakuwa vigumu sana kwa mwanamke kuchukua nafasi hii ya juu katika taifa letu kama iivyojidhihirisha katika teuzi na chaguzi za nyuma.

2) **Uchaguzi wa wabunge na Madiwani**

Tunapendekeza mabadiliko ya kisheria yatakayowezesha kufikia uwakilishi wa 50/50 kwa njia ya majimbo ya uchaguzi ili wanawake wapigiwe kura na wapiga kura wote badala ya kuviachia vyama vya siasa kutumia au kugeuza haki za wanawake kwenye kuteuliwa kama ni jambo la hiari au hisani. Pia tunapendekeza majimbo ya uchaguzi yagawanywe upya kwa kuzingatia wingi wa watu na sio kijiographia. Hii itawezekana endapo Mswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Sura ya Sita itafanyiwa mabadiliko makubwa. Kimantiki wanamtandao tunadai mfumo ulio wazi, huru na salama wenye kuwezesha wanawake kutumia haki zao za msingi za kuchagua, kushindana na kushinda/shindwa. Kimantiki mfumo wa sasa wa viti maalum unakinzana na azma ya kujenga demokrasia shirikiri kwa mrengo wa jinsia kwa sababu zifuatazo:

a) Umejenga daraja na ubaguzi kati ya wawakilishi wa majimbo katika teuzi za nafasi mbalimbali pamoja na stahiki tofauti ikiwa ni pamoja kutoweza kushika au kuteuliwa nafasi ya Waziri Mkuu, Spika wa bunge, kuongoza Baraza la Madiwani pamoja na kutokustahili mfuko wa jimbo kwani jimbo la uchaguzi limetafsriwa kijografia na siyo uwakilishi wa makundi. Ubaguzi huu unakinzana na misingi ya Kikatiba kama ilivyoelezewa kwenye Kifungu cha 21(2 ) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kinachopiga marufuku kwa sheria yoyote iliyotungwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuweka sharti lolote ambalo ni la ubaguzi ama wa athari au kwa taathira yake. Kifungu cha 5 kinatoa tafsiri ya ubaguzi " kubagua maana yake ni kutimiza haja, haki, au mahitaji mengineyo kwa kuzingatia utaifa, ukabila… jinsia.

b) Mfumo huu unawanyima wanawake ushiriki katika kupigiwa kura na raia wote na kuviachia vyama kuteua wawakilishi hawa kwa ajili ya maslahi ya vyama na kwa kutimia mifumo ya uteuzi ambayo haina uwazi

c) Mfumo huu pia unawaweka wanawake katika hatari kubwa ya kupitia vitendo vya unyanyasaji wakati wa michakato kwenye vyama vyao ikiwa ni pamoja na rushwa ya ngono

***Faida za huu mfumo***

i. Kuimarisha demokrasia shirikishi kwa mrengo wa jinsia

ii. Utawajibisha vyama vya siasa kusimamisha wagombea wenye sifa, na kuwawezesha wagombea wao wanawake na wanaume kushinda.

iii. Vile vile mfumo huu hautawabebesha wawakilishi mzigo wote wa gharama za uchaguzi kwani sehemu kubwa ya gharama za uchaguzi zitabebwa na vyama husika, au kwa wagombea binafsi mzigo utabebwa na kundi litakalokuwa linawaunga mkono.

iv. Wawakilishi watakaochaguliwa kwa mfumo huu, watawajibika zaidi kwa wapiga kura wao, ambao hawakulazimika kununua kura zao, bali waliwachagua kwa imani ya ueledi wao katika jimbo husika.

v. Kwa njia hii, rasilimali za uchaguzi zitatumika kwa kuzingatia usawa, tutapunguza rushwa kwenye kuwania uchaguzi, na hatimae taifa litanufaika zaidi kwa kupata wawakilishi waliyo bora na imara.

Ikumbukwe kwamba mabadiliko ya mfumo huu hayakinzani na dhamira ya kuchukua hatua mahususi kuongeza ushiriki wa wanawake katika vyombo vya uwakilishi (affirmative action). Pia wasiwasi ulioko kwamba mfumo utakinzana na matakwa ya katiba hayana mshiko kwani misingi ya katiba imebainisha na kukataza kwa sheria yoyote inayoweka masharti ya ubaguzi wa aina yoyote ikiwa ni pamoja na ubaguzi wa jinsia. Vile vile

katiba inaweza kufanyiwa maboresho madogomadogo kwa wakati mfupi hadi hapo mchakato wa katiba mpya utakapoanzishwa. Pia asiwasi wa kuongezeka kwa wawakilishi hauna mshiko kwani Tume ya Uchaguzi inayo mamlaka ya kugawa upya majimbo ya uchaguzi ili uchaguzi uzingatie zaidi idadi ya watu na siyo ukubwa wa eneo (jiografia). Sheria inaweza kuweka kiwango kipya cha uwakilishi

### 3) Wajibu wa Vyama vya Siasa katika kujenga usawa wa jinsia

Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa, 2023 hauwajibishi vyama kuzingatia misingi ya usawa kwenye uteuzi wa wagombea, wala kuwajibisha vyama kutenga mfuko maalum wa kuwezesha utekelezwaji wa sera ya jinsia, na haviwajibishi vyama kuwa na mfumo wa uwazi kwa kuzingatia utawala bora na wa wazi kwa mrengo wa jinsia.

Tunapendekeza Mswada huu umeongezea kipengele kipya kimoja (10C) kinachovitaka vyama vya siasa kuwa na sera ya jinsia yenye kuonesha program za ujenzi wa uwezo wa wanawake kwenye kushiriki kwenye meza za maamuzi, pamoja na kuweko kwa dawati la jinsia lenye kusimamia utekelezwaji wa sera hizi.

Kwa kuzingatia msingi wa usawa uliyokuweko katika kifungu 6 A (2) cha sheria ya Vyama vya Siasa ya 2019, na kwa kuzingatia ongezeko la kifungu kipya cha `(10C) Sheria iwajibishe vyama vya siasa kuzingatia msingi wa usawa katika teuzi za wote wanaowania nafasi kwenye chaguzi za udiwani na ubunge pamoja na uteuzi kwenye ushiriki wa uongozi kwenye vyama vyao . Tukumbuke kwamba vyama vya siasa vina wajibu mkubwa wa kuwezesha mfumo wa ushiriki wa wanawake kwenye meza za maamuzi kwani vyama ndo vinauwezo mkubwa wa kufungua na kufunga milango yaani nani aingie kwenye kinyang'anyiro cha uchaguzi, nani ashinde, na nani afungiwe milango.

**4) Watendaji Wakuu wa Tume ya Uchaguzi**

Mswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, 2023 haukubainisha msingi wa usawa wa jinsia, haukuzingatiwa katika kuongoza teuzi za watendaji wakuu na katika kuunda kamati mbalimbali. Pia Mswada haukuwapa watendaji wakuu jukumu la kusimamia chaguzi zote kwa mrengo wa jinsia kama ilvyobainishwa katika mswada wa sheria ya vyama vya siasa kifungu 10C. Tunapendekeza Mswada huo ufanyiwe maboresho ili ubainishe misingi ya usawa wa jinsia kwenye teuzi za watendaji wakuu, kamati husika na kwenye majukumu ya Tume kwenye kusimamia mchakato wote wa uchaguzi. Vile vile kwenye ripoti za Tume kuhusu mwenendo wa uchaguzi ripoti itoe masuala ya jinsia yaliyojitokeza ikiwa ni pamoja na ukatili wa jinsia, ubaguzi na suala zima la wanawake kufikia na kutumia rasimilali za uchaguzi. Ripoti za uchaguzi zikibainisha ukatili wa kijinsia uliojitokeza kwenye uchaguzi husika, kutawezesha vyama vya siasa, mashirika ya kiraia, na tume yenyewe kuchukua hatua kukomesha ukatili wa jinsia katika chaguzi zinazofuata

## HITIMISHO

Sisi Mtandao wa Wanawake, Katiba, Uchaguzi, na Uongozi tunatoa **wito** kwamba:

(i) Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambayo ndiyo imepokea maoni ya raia, asasi, na mashirika ihakikisha inayaingiza mapendekezo yetu kwenye miswada hiyo mitatu kabla ya kuiwasilisha Bungeni kusomwa kwa mara ya pili (Second Reading) ili sheria zitakazotungwa kutokana na miswada hiyo ziwe na misingi ya usawa wa jinsia .

(ii) Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania linayoongozwa na spika mwanamke, ikiwa ni taasisi nyeti kwenye kutunga sheria, ipokee maoni yetu na kuyaingiza kwenye maboresho ya miswada hiyo mitatu; Mswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani,2023, Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa, 2023, na Mswada wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, 2023

**MWISHO**

*Tamko hili limetolewa na Wanamtandao siku ya Jumatatu tarehe 22/01/2024*